Kitabu cha Nabii Yeremia

UTANGULIZI

Alama mojawapo ya wazi katika kitabu cha Yeremia ni maelezo mengi kuhusu maisha ya mwandishi wake binafsi. Sawa sawa na manabii wengine, Yeremia alijua kwamba, kama angetangaza ujumbe wa Mungu kwa uaminifu, watu wengi wasingempenda, lakini maandiko yake yanadhihirisha mahangaiko yaliyotokea moyoni mwake. Alisikitika juu ya hali ya watu wasiomjali Mungu, naye bila kukoma alilaumu desturi mbaya za kidini, tabia mbaya katika jumuia na matendo ya kipumbavu ya serikali katika nchi yote. Adha mbaya aliyopata ilimkatisha tamaa kiasi cha kutosha, lakini kilichomkatisha tamaa zaidi ilikuwa wasiwasi kwamba Mungu hakumtendea vizuri.

Tukitaka kuelewa ugumu na matatizo yaliyomkabili Yeremia, ni lazima tuelewa kwanza hali ya watu aliowahubiria. Kabla ya miaka mia moja hivi, ufalme wa kaskazini (wa Israeli) uliangamizwa, na watu wake walitawanywa katika mataifa ya ufalme wa Uashuru. Wakati huo ufalme wa kusini (wa Yuda) ulikabiliwa na hukumu iliyofanana, na ilikuwa kazi ya Yeremia kuwaonya watu wasiotaka kutubu na kuwaambia kwamba siku ya hukumu yao ilikaribia sana.

MAZINGIRA YA KIDINI

Marekebisho ya mfalme Yosia

Wakati wa utawala wa Yosia (miaka ya 640 hadi 609 k.K.) marekebisho ya dini ya Wayuda pamoja na uamsho wa huduma safi ya manabii vilikuwepo katika taifa zima. Mtu aliyeanzisha marekebisho hayo alikuwa Yosia mwenyewe, na mtu mashuhuri zaidi wa uamsho wa huduma ya unabii alikuwa Yeremia. Yosia aliporithi kiti cha enzi cha Yuda, alirithi nchi ambayo dini na maadili yake viliharibika vibaya. Wafalme wawili waliotawala kabla ya Yosia, yaani Manase na Amoni, walikuwa wametawala muda wa miaka 57, na katika muda huo walisababisha watu wa Yuda waabudu miungu ya kigeni na kuchafuka kimaisha kuliko mataifa mengine ya Kikanaani yaliyoangamizwa na Mungu kwa sababu ya makosa yao. Mfalme Manase aliingiza desturi za dini za kigeni za kila aina. Pia alianzisha siasa ya kitaifa iliyothibitisha desturi hizo badala ya ibada ya kweli ya BWANA (2Fal 21:1-9; 16:19-22). (Hata Amoni alifuata siasa hiyo.) Yosia alipoimarika sawa sawa katika ufalme wake, alifanya mikakati ya kuleta marekebisho katika Yuda, akiwa na makusudi ya kuondoa desturi hizo zote za kigeni na kuimarisha ibada ya BWANA (YAHWEH) tena kama ilivyofundishwa na Musa.

Kizazi kipya kilichozaliwa wakati wa miaka 57 ya enzi za wafalme Manase na Amoni kilikuwa na ufahamu mdogo kabisa kuhusu sheria ya Mungu aliyowapa Waisraeli katika Mlima Sinai. Mafundi walipofanya ukarabati katika hekalu, waliona baadhi ya magombo ya sheria yaliyosahauliwa tangu muda mrefu, na hivyo Yosia aliweza kuyasoma. Alishtuka sana aliposoma jinsi watu wa Yuda walivyokwenda mbali na mapenzi ya Mungu, lakini jambo hili lilizidisha nia ya mfalme kutekeleza matengenezo yake ya dini. Aliwaondoa makuhani wote wa ibada ya sanamu na kuharibu mahali pa ibada hiyo pamoja na vitu vingine vilivyokuwepo kwa ajili ya heshima ya miungu ya kigeni. Aliingiza upya sherehe ya sikukuu ya Pasaka, akaleta ibada yote ya BWANA Yerusalemu na kupiga marufuku aina yo yote ya ibada ya mizimu (au mahoka) na ubashiri wa kichawi (2Fal 22:1-23:25).

Lakini matengenezo ya Yosia hayakutosha kuondoa kabisa mawazo ya ibada ya miungu yaliyoota mizizi mikubwa katika mioyo ya watu. Ingawa machafuko ya kidini yaliondolewa na kanuni safi za dini ziliingizwa, watu wachache tu walibadilika mioyoni mwao. Taifa kwa jumla bado lilimwasi Mungu nalo lilielekea hukumu ya Mungu. (2Fal 23:26-27).

Yeremia alivyoona dini ya Wayuda

Katika mwaka wa 627 k.K., yaani wakati wa utawala wa Yosia, Yeremia alianza huduma yake ya unabii (Yer 1:1-2). Lakini Yeremia alitaja marekebisho ya Yosia kwa nadra sana. Akiwa nabii, aliona kwamba hayakuwepo mabadiliko ya mioyo ya watu, kwa hiyo mabadiliko ya desturi za nje za dini hayangekuwa na matokeo ya kudumu (Yer 9:25-26; 11:15). Kwa kweli, ibada ya sanamu za miungu haikuchelewa kurudi tena (Yer 7:16-20; 19:3-9).

Yeremia hakutaka kumkatisha tamaa mfalme aliyefanya bidii katika kazi yake njema, lakini alijaribu kuchimba chini zaidi katika mioyo na dhamiri za watu. Hakupinga uamsho na marekebisho ya mipango ya sadaka na ibada, kwa sababu utii wa sheria ya Musa ulitakiwa sana (Yer 17:21-22, 26); lakini alitia mkazo kwamba, kama watu wasingeamshwa kiroho na kiadili, kwa hakika wangeanguka chini ya hukumu ya Mungu (Yer 14:12).

Baada ya kufa kwake Yosia, Yeremia aliingia katika wakati wa maana zaidi ya kazi yake. Maonyo

yake yalikuwa na mkazo zaidi alipowahakikishia watu kwamba, kwa sababu ya kudumu kwao katika tabia na maisha yao, wangepelekwa kifungoni Babeli (Yer 10:17-18; 21:2-7; 26:1-6).

Mjumbe wa Mungu aliyekataliwa
Watu hawakupenda kusikia matangazo ya Yeremia ya kila wakati kwamba Wababeli wangeteka Yerusalemu, wangebomoa hekalu na kuwapeleka watu kifungoni. Matokeo yake, Yeremia aliudhiwa siku zote za maisha yake. Alipingwa sana na jamaa zake mwenyewe (12:6), na watu wa mji wake alipokulia (11:19-21), na wenyeji wa Yerusalemu kwa jumla (15:10,20; 18:18; 20:7), na viongozi wa dini (20:1-2; 28:10-11; 29:24-28), na watawala wa kiraia (37:11-15; 38:1-6, 24-27) pamoja na wafalme wenyewe wa Yuda (36:26; 37:18). Alipigwa (20:2; 37:15), mara nyingine alifungwa gerezani (20:1-2; 37:15, 21; 38:13) na mara nyingi alitishwa kuuawa (11:21; 26:7-9; 36:19, 26; 38:4,15).

Yeremia hakuoa (16:2), na kwa muda mrefu wa maisha yake alikuwa na marafiki wachache sana. Watu wengi zaidi wa jumuia hawakupenda kuchangamana naye (15:10,17), na baada ya muda alikatazwa hata kuingia hekaluni (36:5). Ukiwa wake ulizidi tena alipokatazwa kushiriki katika mambo ya kawaida ya jumuia kama vile karamu za watu au mazishi (16:5,8). Lakini walikuwepo watu wachache wenye vyeo vya juu ambao mara nyingine waliweza kumpatia ulinzi fulani dhidi ya watesi wake (26:24; 38:7-13; 40:5-6).

MAZINGIRA YA HISTORIA
Habari ya kuwa unabii mbalimbali ulioandikwa katika kitabu cha Yeremia haukupangwa kwa mfululizo wa matukio ya historia, mara nyingine inaweza kumhangaisha msomaji. Ili kusaidia kuelewa kitabu vizuri zaidi, muhtasari unaofuata unatoa utaratibu wa matukio ambayo hutoa mazingira ya ujumbe mbalimbali wa Yeremia.

Kuharibika kwa mamlaka ya Uashuru
Jambo mojawapo lililomsaidia mfalme Yosia katika matengenezo yake ya dini lilikuwa kupungua kwa mamlaka ya Uashuru ambao mpaka wakati huo ulikuwa utawala mkuu katika eneo lile lote. Kabla ya miaka mia moja hivi Waashuri walikuwa wameangamiza ufalme wa Israeli uliokuwa wa udugu wa Yuda (2Fal 17:5-6). Waashuri hao pia walikuwa wamefanya maisha ya wafalme wa Yuda kuwa magumu (taz. maelezo yanayotangulia kitabu cha Isaya). Udhaifu wa mamlaka ya Uashuru wakati wa Yosia ulitosha kwa kumwezesha Yosia kutekeleza marekebisho katika nchi yake bila ya kuingiliwa na maadui wajirani.

Mamlaka ya Waashuri yalipopungua, Wababeli na hata Wamisri walizidi kupata nguvu katika eneo lile. Wababeli walipoteka mji mkuu wa Uashuru, Ninawi, mwaka wa 612 k.K., Farao Neko (Necho), mfalme wa Misri, aliondoka ili azuie utekaji wa Wababeli. Labda alitumaini kwamba angeweza kuimarisha maeneo ya magharibi yaliyobaki katika Uashuru, kusudi apate kizuizi cha eneo la kujitetea kati ya Misri na Babeli.

Kwa kuwa nchi ya Yuda ilikuwa katikati ya maeneo ya Uashuru na Misri, mfalme wa Yuda, Yosia, aliona mwungano ule wa Uashuru na Misri kuwa ni hatari kwa uhuru wake mwenyewe. Akipendelea Uashuru uendelee kuwa dhaifu, aliamua kuzuia majeshi ya Farao yaliyopita Palestina katika njia yake ya kuelekea Uashuru. Uamuzi huo ulitokea kuwa kosa kubwa mno. Wayuda walishindwa, na Yosia aliuawa vitani (mwaka wa 609 k.K.; 2Fal 23:28-30). Wakati huo Uashuru haukuweza kuendelea kujitetea dhidi ya Wababeli nao ukaanguka. Ukaingizwa katika ufalme wa Babeli wala haukuendelea kuwa taifa.

Mwisho wa uhuru wa Yuda
Baada ya kufa kwake mfalme Yosia, watu wa Yuda walimfanya mwana wa pili wa Yosia, Yehoahazi, kuwa mfalme wao mpya (2Fal 23:30). Lakini wakati huo Farao Neko alijiona kuwa mtawala wa Yuda, naye hakupenda kumkubali mfalme aliyechaguliwa na watu. Alimchukua Yehoahazi kuwa mfungwa wake huko Misri na badala yake alimweka kaka yake, Yehoyakimu, katika kiti cha enzi. Kisha akadai kodi nyingi sana kwa Wayuda (2Fal 23:31-34).



Baada ya muda mfupi wa utawala wa Yehoyakimu ilionekana wazi kwa nini watu hawakumchagua yeye kuwa mfalme. Alikuwa mfalme katili, mwenye kiburi naye aliwanyanyasa watu, kwa kweli hakukawia kumwua mtu ye yote aliyethubutu kumpinga au aliyemkasirikia kidogo tu (2Fal 24:4; Yer 26:20-23; 36:21-26). Ingawa nchi yake ilidaiwa kodi nyingi sana na Wamisri, mfalme binafsi alijijengea majumba makubwa ya kifalme yenye fahari nyingi, akiwalazimisha mafundi wa ujenzi wafanye kazi yake bila malipo yo yote (Yer 22:13-18).

Mwanzo wa utekaji wa Babeli
Katika vita vikali baina ya Misri na Babeli Wababeli waliwashinda Wamisri katika mashambulio makali yaliyojulikana kuwa ya Karkemishi, mwaka wa 605 k.K. (Yer 46:2). Maana ya ushindi huo ilikuwa kwamba, tangu wakati huo Yuda ilikuwa chini ya utawala wa Babeli, nayo ilipaswa kuwalipa Wababeli kodi badala ya Wamisri.

Washindi wa jeshi la Babeli waliporudi kwao, walichukua pamoja nao wafungwa vijana wenye uwezo na elimu ya juu walioweza kuwapata katika nyumba za wakuu wa Yerusalemu. Vijana wale, miongoni mwao walikuwa Danieli na marafiki zake watatu, walipelekwa ili wafundishwe kazi ya utawala katika serikali ya Babeli (Dan 1:1-6).

Baada ya miaka mitatu, Yehoyakimu aliwaasi Wababeli akikataa kuendelea kuwalipa kodi. Uamuzi huo ulikuwa wa hatari sana, lakini Yehoyakimu alitumaini kwamba mfalme wa Babeli, Nebukadreza, alishughulika zaidi na vita vya sehemu nyingine, hata asiweze kujali maasi ya nchi ndogo ya mbali kama Yuda. Ingawa Nebukadreza hakushambulia Yerusalemu mara hiyo, hakuisahau. Siasa yake ya kuchukia Yuda ilikuwa kuhamasisha mataifa ya jirani yaliyokuwa chini ya utawala wake kuingia na kuiba katika nchi ya Yuda, na hivyo pole pole alidhoofisha nchi hiyo kwa habari ya uchumi, siasa na kijeshi (2Fal 24:1-2).

Hivyo baada ya kushinda maasi ya sehemu nyingine, Nebukadreza alituma majeshi yake ili yazingire Yerusalemu kivita. Inaonekana kama wakati huo wenyeji wa Yerusalemu walichoka kumvumilia mfalme wao mbaya, Yehoyakimu, wakamtoa na kuwapa Wababeli, ili wapate masharti mazuri kwa ajili yao wenyewe. Ingawa jiji lilikuwa bado halijatekwa, Yehoyakimu alikamatwa na maadui. Alifungwa kwa minyororo tayari kwa kupelekwa Babeli, lakini kabla ya kuanza safari yake alikufa. Hakuna mtu aliyemsikitikia, na maiti yake ilitupwa katika jalala la takataka nje ya Yerusalemu kana kwamba ilikuwa mzoga wa mnyama mchafu (2Nya 36:6; Yer 22:18-19; 36:30).

Yekonia (au Yehoyakini au Konia) alitawazwa kuwa mfalme alipokuwa na umri wa miaka 18 tu, lakini

baada ya miezi mitatu tu aliona kwamba hakuweza kuendelea kujitetea dhidi ya Wababeli. Kwa hiyo alijisalimisha kwa Wababeli akitumaini kwamba angeweza kupunguza shida za Yerusalemu na kutendewa mema na washindi wake (mwaka wa 597 k.K.; 2Fal 24:10-12).

Baada ya kushinda Yerusalemu, Wababeli walipunguza hatari ya uasi jijini kwa kuchukua karibu mali yote pamoja na watu wenye sifa nzuri kifungoni Babeli. Waliwaacha watu wale tu wasioweza kuwafaa kitu wakamchagua Sedekia (baba mdogo wa Yekonia, yaani mwana mwingine wa Yosia) na kumweka kuwa mfalme wao (2Fal 24:12-17).

Kubomolewa kwa Yerusalemu
Sedekia alikuwa mfalme dhaifu aliyekubali mashauri ya watu wo wote walioweza kumshawishi kidogo. Baada ya viongozi wenye uwezo kupelekwa Babeli, Sedekia alitegemea msaada wa washauri waliotafuta faida yao binafsi tu, na uwezo wao wa siasa ulikuwa finyu wala mambo ya kidini hawakuelewa. Daima walijaribu kumhamasisha Sedekia atafute msaada wa Wamisri ili wawaasi Wababeli. Lakini Yeremia hakuacha kupinga mipango yo yote ya kuasi Babeli, kwa sababu aliona kwamba mambo hayo yangeleta maafa na matisho tu pamoja na kubomolewa kwa Yerusalemu. Ushauri wake daima ulikuwa kwamba, Wayuda wakubali hali yao ya kutii Babeli kuwa mapenzi ya Mungu (2Fal 24:18-20; Yer 21:1-10; 27:12-22).

Kwa ujinga wake, Sedekia alifuata ushauri wa watu waliopendelea Misri akawaasi Wababeli. Nebukadreza akakasirika akaamua kukomesha uasi wa Yuda moja kwa moja akatuma majeshi yake, ili katika mashambulio ya mwisho yabomoe Yerusalemu kabisa. Wamisri walipofika ili wawasaidie Wayuda, mazingira ya kivita yaliondolewa Yerusalemu kwa muda, lakini Yeremia aliwahakikishia wenyeji kwamba Wababeli wangerudi hakika nao wangeponda Misri pamoja na Yuda. Chama cha kupendelea Misri kikamshtaki Yeremia kuwa msaliti kikampiga na kumfunga gerezani (Yer 37:1-21).

Baada ya muda mfupi tu, Wababeli walirudi na unabii wa Yeremia ulionekana kuwa kweli. (Vitisho vya kuzingirwa Yerusalemu wakati huo vinaelezwa vizuri katika kitabu cha Maombolezo.) Mwisho wake Wababeli walipobomoa ukuta wa jiji sehemu moja, Sedekia pamoja na baadhi ya watu wake walijaribu kutoroka, lakini walikamatwa na maadui (2Fal 25:1-7).

Katika ushindi wao, Wababeli waliteka Yerusalemu yote, wakichukua kila kitu kilichokuwa na thamani yo yote na kilichoweza kuchukuliwa Babeli. Pia waliteketeza au kubomoa vitu vyote vilivyobaki. Waliwaua viongozi wa uasi wakawafanya wenyeji wengine kuwa wafungwa isipokuwa wachache wasiofaa kabisa. Walimtoa Yeremia gerezani na kumpa uhuru wa kuchagua sehemu ya kuishi, Babeli au Yuda. Yeremia akaamua kuishi Yuda pamoja na wakulima wachache na watu wengine wa hali ya chini kabisa wasiowafaa Wababeli (2Fal 25:8-21; Yer 39:13-14; 40:4-6). Huo ulikuwa mwisho wa Yerusalemu (mwaka wa 587 k.K.).

Yeremia apelekwa Misri
Gedalia, mmojawao wa viongozi wachache wasiopenda siasa ya Sedekia ya kupendelea Misri, aliwekwa na Wababeli kuwa mtawala wa watu wachache waliobaki Yuda. Kwa msaada wa Yeremia, alifuata siasa ya Babeli. Hakuchukua hatua dhidi ya baadhi ya viongozi wa kijeshi wa Yuda walioweza kutoroka katika jeshi la Wababeli. Badala yake aliwakaribisha pamoja na wakimbizi wengine waliokuwa wamejificha nje ya nchi, ili warudi na kuishi karibu na Yerusalemu (2Fal 25:22-24; Yer 40:7-12).

Lakini watu wale waliopinga Babeli walikuwa bado hawajajifunza mambo ambayo Yeremia alijaribu kuwafundisha. Wakikataa utawala wa Wababeli, walimfitini mtawala aliyewekwa nao , yaani Gedalia, na ilipotokea nafasi nzuri walimwua Gedalia. Wayahudi hao waliobaki nchini waliogopa mashambulio ya kisasi ya Nebukadreza, wakakimbia kwenda Misri kwa usalama wao wakamchukua Yeremia kwa nguvu, ingawa alijaribu kukataa (2Fal 25-26; Yer 40:13-43:7).

Hata huko Misri, katika nchi ambayo msaada wake siku zote alikuwa amekataa, Yeremia aliendelea kutoa ujumbe wa Mungu. Lakini watu wa Mungu walikataa kutii ujumbe huo (Yer 43:8-44:30). Kufuatana na masimulizi ya mapokeo ya Wayahudi, watu wale walimkasirikia sana Yeremia na mwisho walimwua kwa mawe.

Matumizi ya majina
Wakati wa kugawanywa Israeli katika falme mbili, Biblia inaita ufalme wa kaskazini Israeli (au mara nyingine Samaria, kufuatana na mji wake mkuu), na ufalme wa kusini uliitwa Yuda (au mara nyingine Yerusalemu, kufuatana na jina la jiji kuu la kusini). (Kwa maelezo zaidi taz. utangulizi wa kitabu cha

Isaya.) Wakati wa unabii wa Yeremia, ufalme wa kaskazini, yaani wa Israeli, ulikwisha tekwa na Waashuri, na watu wake walipelekwa katika nchi nyingine. Ufalme wa kusini tu, yaani wa Yuda, ulibaki. Yeremia mara nyingine anatumia jina Israeli anaposema habari za Yuda, kwa sababu anatumia neno hilo kadiri ya matumizi yake ya kale na kwa maana ya jumla wala siyo kadiri ya matumizi yake wakati wa ugawanyo wa ufalme.

Lakini kwa kuzuia kuhangaishwa, maelezo yetu ya kitabu hiki yanataja ufalme wa kusini kwajina la Yuda tu. Jina la Israeli linatumiwa pale tu linapotaja habari za ufalme wa kaskazini, isipokuwa maelezo ya jumla yanaonyesha wazi kwamba jina hilo linahusika na Israeli ya kale (k.v. Israeli ya wakati wa Musa).

MUHTASARI

1:1-6:30	Muda wa kwanza wa huduma ya Yeremia
7:1 -20:18	Hali ya kiroho katika Yuda
21:1-25:38	Maonyo kwa wafalme na manabii wa uongo
26:1-34:22	Unabii kuhusu kifungo na kupewa uhuru tena
35:1-45:5	Matukio katika Yuda na Misri
46:1 -51:64	Ujumbe kwa mataifa ya kigeni
52:1-34	Nyongeza za historia